

South Carolina Department of Social Services
TAARIFA YA MASIKILIZO YA HAKI

Unaweza Kukata Rufaa na Upate Masikilizo ya Haki

Ikiwa hukubailiani na manufaa unayopata kutoka kwetu, au ikiwa manufaa yako yamekataliwa au kusimamishwa, unaweza kuitisha Masikilizo ya Haki. Katika Masikilizo ya Haki wewe na DSS mutamuambia Ofisa wa Masikilizo kilichofanyika katika kesi yako. Kisha Ofisa Msimamizi wa Kusikilizwa atakutumia uamuzi wa kesi yako.

Jinsi ya Kuitisha Masikilizo ya Haki

Unaweza kupiga simu kwa 1-800-311-7220 au uandika barua kwa ofisi yako ya karibu ya DSS upate Masikilizo ya Haki. Usisubiri zaidi ya siku 90 kuanzia tarehe ya notisi hii kupiga simu au kuandika barua kwa DSS kuitisha Masikilizo ya Haki kuhusu SNAP yako. Usisubiri zaidi ya siku 60 kuanzia tarehe ya notisi hii kuitisha Masikilizo ya Haki kuhusu Uhuru wa Familia (FI) yako. Ambia DSS ikiwa una mahitaji maalum au ikiwa unahitaji mkalimani au nyenzo zilizotafsiriwa.

Unahitaji Mwakilishi?

Unaweza kujitetea mwenyewe katika Masikilizo ya Haki. Pia unaweza kuja na rafiki, jamaa, au wakili (kwa gharama yako) azungumze kwa niaba yako. Unaweza kupata msaada wa kisheria bila malipo kutoka kwa ofisi ya Msaada wa Kisheria au Huduma za Kisheria iliyo karibu kwa kupiga simu kwa 1-888-346-5592 kutoka jimbo zima au 803-744-9430 ukiwa katika eneo la Kolumbia (Msaada wa Kisheria au Huduma za Kisheria sio sehemu ya DSS).

Tunasimamisha au Kupunguza Manufaa Yako?

Ikiwa unataka kupokea manufaa ya kuendelea, lazima uitishe Masikilizo ya Haki na uchague Masikilizo ya kuendelea ndani ya siku 10 kuanzia tarehe ya barua hii. Ikiwa siku ya 10 ni wikendi au sikukuu, unaweza kuitisha siku inayofuata ya kazi. Ikiwa utaitisha kusikilizwa na manufaa ya kuendelea ndani ya siku 10, utaendelea kupata manufaa sawa hadi uamuzi wa kusikilizwa. Ikiwa unashiriki katika Programu ya Kazi ya FI, lazima unedeele kushiriki katika shughuli ya programu ya kazi ili upokee manufaa ya kuendelea ya FI. Ikiwa uamuzi utakuwa kinyume na ulichotaka, huenda ukahitajika kuyarudisha. Hatuwezi kuendeleza manufaa yako ya SNAP ikiwa kipindi chako cha cheti cha SNAP kitakwisha kabla ya Masikilizo ya Haki. Ukiitisha Masikilizo ya Haki kwa sababu ya kufungwa kwa kesi ya miezi 24 hutapokea manufaa ya kuendelea. Ikiwa utasubiri zaidi ya siku 10 ili kukataa rufaa, bado unaweza kupata Masikilizo ya Haki, lakini hatutaendeleza manufaa uako.

Baada ya Masikilizo ya Haki

Ikiwa uamuzi wa Masikilizo ya Haki utakuwa unavyotaka, huenda ukapokea kiasi cha manufaa au manufaa yote yaliyosimamishwa au kukatwa. Ikiwa uamuzi utakuwa kinyume na ulichotaka na umepokea manufaa ya kuendelea, huenda ukahitajika kuyarudisha. DSS huenda ikashikilia sehemu kidogo ya usaidizi wowote unaopokea wa SNAP au Usaidizi wa Famili ili kulipa unachodaiwa.

Kumbuka: DSS itakujulisha wakati wa kuendeleza manufaa yako ya SNAP au FI. **Ili uendeele kupokea manufaa kutoka kwa DSS bila kukatizwa**, rudisha cheti chako kipya au fomu ya uamuzi mpya na taarifa kwa ofisi yako ya DSS ili iendeeleze manufaa yako ya SNAP au FI **kabla** manufaa yako yasimamishwe.

Kumbuka: Ni wajibu wako kujulisha DSS kuhusu mabadiliko fulani katika familia yako. Unaweza kuripoti mabadiliko haya kwa kuandika barua, kwa kupiga simu kwa ofisi yako ya DSS au kwa kutumia DSS 1620 Ripoti ya Mabadiliko ya Kitoa Ripoti Rahisi (ya SNAP) au DSS 12117 Fomu ya Kuripoti Mabadiliko – Wapokeaji wa Manufaa/Huduma Huru za Familia (ya FI).